

UJASIRI NI NGUVU YA KUTUVUSHA KATIKATI YA HATARI

MAANDIKO: MITH. 28:1, EBR. 10: 35 – 39

UTANGULIZI:

- Mungu anaposema msiutupe ujasiri wenu ni kwa sababu anajua kuwa wako watu wanaoanza vizuri lakini siku zinavyoendelea wanalegeza msimamo taratibu na kumaliza vibaya mf ni Assa na Samsoni **2Nyak 14-16, Amuz 13-16**
- Haijalishi tunapita katika hatari na misukosuko kiasi gani bado Mungu anataka kujisazia watu mashujaa- **1Falm. 19:18.** Siri ya ushindi wetu ni kuwa na moyo waujasiri katika hayo yote, Mungu hana furaha na mtu wa kusitasita, kulialia na kukata tamaa anataka usonge mbele bila kuangalia vikwazo – **kut. 14: 10-18.**

Hatari – ni hali ya **kutokuwa katika usalama, hali inayoleta fadhaa, uharibifu, vitisho, maafa** n.k.

Maana ya ujasiri - ni uhodari, ushujaa.

- **Hi hali ya kukabili jambo gumu bila hofu.**
- Ni uwezo ulio ndani ya mtu kutokana na anachokiamini unaomwezesha kufanya maamuzi magumu ambayo wengine wanaogopa kufanya – *1Samwl. 17: 31 – 37; 43 – 50*
- **Fikiria sikku 40 Mfalme Sauli na jeshi lake na Israeli** wote wanamkimbia Goliathi lakini Daudi kijana mdogo ambaye moyo wake una mtumaini na kumwamini Mungu anainuka kishujaa kwenda kupigana
- **Kinyume cha ujasiri ni woga, wasiwasi mashaka na kukata tamaa- miongoni mwa silaha kubwa anazotumia shetani ili kuwakosesha watu ni woga – Hes. 14:1-4 (13: 31-33) - habari mbaya, Waam. 7: 2 -3- tangazo - waoga warudi nyumbani.**
- **2Tim. 1:7 – Mungu hakutupa roho ya woga bali ya nguvu – woga unatoka kwa shetani**
- Mkristo halisi atajulikana wakati wa majaribio ya Imani, Ukristo usiogharimu kitu chochote hauna thamani yoyote. **Math.10: 34– 39.**
- **Mungu anapendezwa na mtu mwenye uwezo wa kusimama imara katikati ya upinzani.**

- **Mikaya- 1Falm. 22: 1 - 28** alisimama imara katikati ya manabii wa uongo na mfalme Ahabu – **(mst. 12)**
- **Paulo** - anasema **hatulegei** tumekataa kulichanganya neno la Mungu na uongo.- **2Kor. 4: 1-6**
- **Je sisi tunaweza kuitetea Injili ya kweli ya Yesu Kristo katika kizazi hiki kilichoharibika?** Au tunachukuliana na watu kwa hekima za binadamu, Mungu atusaidie.
- **Daudi** katikati ya hatari ya kuuawa na maaskari wake hakukata tamaa – **akajitia nguvu katika Bwana** – akauliza kwa Bwana akapata majibu sahihi – **1Samwl. 30: 1 – 20 (mst. 6,8)- Daudi hakuweka uadui kwa wale watu aliwachukua kwenda nao kupigana na Waamaleki, na wakapata ushindi wa kishindo.**
- **Yehoshafati** katikati ya hatari - majeshi yamejipanga tayari kuja kupigana naye **anachukua hatua ya kuwakusanya watu kwenda kuomba** - ingekuwa ni leo Mfalme angepanga majeshi chap chap kwenda vitani, kumbe katika vita hii Mungu alitaka apigane mwenyewe – **2Nyakat. 20: 1 – 30 (mst. 15 – 19)**
- **Mwanamke Mshunami** – Jamani alikuwa jasiri – fikiri mtoto wa pekee amekufa - Halii, wala hapigi kelele, hamwelezi mmewe wala mfanyakazi – anapiga mbio kwenda kwa Mtummishi wa Mungukumweleza shida yake – Je sisi tunaweza? – **2Falm. 4: 8 - 37, (18 – 28)** - ee Yesu tupe moyo wa ujasiri.
- **Ester na Mordekai-** Katikati ya hatari ya Wayahudi wote kuuawa kutokana na msimamo thabiti wa Mordekai kukataa kumsujudia Hamani, Mordekai anajitolea kufunga na kuomba na kumjulisha Esta madhara yanayowakabili Wayahudi wote kisha Esta anamtuma Mordekai waende kufunga na kuomba siku 3 kisha ataingia kwa Mfalme kinyume cha sheria kama ni kuangamia yuko tayari. **Esta 4: 1 – 17 (15 – 17)**

- Ujasiri wa Esta kuwa tayari kuangamia ulimtengenezea kibali kikubwa kwa Mfalme na adui yao Hamani akauawa - watu wa Mungu wakatawala - **soma sura 5-8.**
- **Hata siku moja Mungu hafanyi kazi na watu waoga. Usalama wa Taifa letu unatutegemea sana.**

Nini kinatupa ujasiri?

1. **Ufahamu wetu juu ya Mungu na nguvu zake – Dan. 11: 32, Ayub. 22:21.**
 - Wakati ulimwengu unaweweseka na kukata tamaa ni wateule pekee wamjuao Mungu wao wawezao kusimama kwa ujasiri na kuudhirisha uwezo wa Mungu wao.
 - **Mjue sana Mungu ili uwe na amani** – akina Daniel na wenzake katikati ya tanuru la moto, ndani ya tundu la samba walitulia, kwa sababu walimjua waliyemwamini. **Dan 3 na 6**
 - **Paulo na Sila** ndani ya gereza pamoja namapigo mengi na kufungwa kwa mkatale waliendelea kumwomba na kumsifu Mungu Bwana akashuka kuwatetea. **Mdo. 16: 19 - 26**
2. **Jitihada binafsi katika kumtafuta Mungu na kujazwa nguvu za Roho Mtakatifu nyakati zote. Zab 105:4, Mdo. 6:8-10, Zab. 119:11**
 - Washindi wote ambao tumewasoma hapo juu walikuwa watu wa maombi. Kumjua Mungu bila kujaa nguvu zake haitatusaidia kitu lazima ujitahidi kuwa mtu wa maombi na lbada siku zote.

Kwanini tuombe ujasiri?

1. Biblia inaeleza wazi kuwa **siku za mwisho zitakuwa siku za hatari** mashujaa tu ndio watakaopenya **2Tim 3, Math 24**
2. **Unachoogopa ndicho kitakachokujia- Mith 10:24** woga ni dalili ya kutomjua Mungu, na kutomwamini hivyo unafungulia mashetani mlango wa kukutesa na kukutawala. .
Mbarikiwe na Bwana.

Dr. A. L. Mwizarubi (Mrs)
SAYUNI EAGT – ARUSHA
3/10/2021